



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA

(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Unapojibu tafadhali taja;

Kumb. Na CDC/I.20/VOL 1/39

03/05/2023

TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA YA HALMASHAURI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba anapenda kuwataarifu Wananchi wote wakazi wa Chemba wenye sifa kuomba na kuwasilisha maombi yao ya nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri.

2. SIFA ZA MWOMBAJI.

- i. Awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.
- ii. Awe na umri kuanzia miaka 45 na kuendelea.
- iii. Awe na taaluma ya Utawala, Sheria au Uongozi.
- iv. Awe Mwadilifu.
- v. Awe na uzoefu wa masuala ya uongozi.

3. MAJUKUMU YA BODI.


- i. Kufanya uteuzi wenye tija wa wafanyakazi na kuwasilisha mapendekezo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa taratibu za uteuzi kama zilivyoainishwa katika kanuni.
- ii. Bodi itazingatia miongozo ya Utumishi wa Umma iliyoteuliwa na Tume pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
- iii. Itazingatia Kanuni za usawa na uwazi katika uteuzi wa Wafanyakazi na kujiepusha na ushawishi wa mtu yeyote nje ya bodi.
- iv. Bodi itazingatia Kanuni za usawa wa fursa kwa wote ikiwa ni pamoja na usawa wa kijinsia.

v. "Function of the Board shall be to conduct merit – based selection of ataff and submit proposals to the Local Government Authority Concerned as part of the appointment procedures set out in these regulations"

Barua za maombi ziwasilishwe pamoja na nyaraka zifuatazo:-
CV, Vyeti vya Taaluma na Utaalamu na Cheti cha kuzaliwa kwa anuani ifuatayo:

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA,
S.L.P 830,
CHEMBA.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 30/5/2023 saa 9:30 mchana



SIWEMA H. JUMAA
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
CHEMBA.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
CHEMBA